# **KANUNI ZA UVUVI (**Kundi La Usimamizi Wa Ufuo**), 2007**

MPANGILIO WA VIGAWANYIKO (SEHEMU)

SEHEMU YA KWANZA- UTANGULIZI

*Sehemu*

1. Dondoo
2. Tafsiri/Maelezo
3. Malengo
4. Muundo wa utawala
5. Eneo la mamalaka ya Kundi La Usimamizi Wa Ufuo
6. Sheria za maelekezo
7. Ushirikiano wa usimamizi
8. Ulinzi wa mazingara

SEHEMU YA TATU: uanachama na uchaguzi wa Kundi La Usimamizi Wa Ufuo

9. Uanachama
10. Vigawanyo vya uanachama
11. Utaratibu wa kujiunga
12. Kujiuzulu na kutolewa kwenye kundi la Kundi La Usimamizi Wa Ufuo
13. Haki na majukumu ya wanachama wa Kundi La Usimamizi Wa Ufuo
14. Kamati tendaji
15. Kuchaguliwa kujiunga na kamati tendaji
16. Kuundwa na kuchaguliwa kijiunga na kamati ndogo

SEHEMU YA IV: Usimamizi wa Kundi La Usimamizi Wa Ufuo

17. Mikutano ya wanachama wa Kundi La Usimamizi Wa Ufuo
18. Kongamano la bunge
19. Mikutano ya kamati tendaji
20. Kuachishwa uanachama wa kamati tendaji na bunge
21. Kusimamishwa kwa kamati tendaji na mkurugenzi
22. Waajiriwa wa Kundi La Usimamizi Wa Ufuo

SEHEMU YA V: Majukumu ya vikundi maalum na maafisaa wa Kundi La Usimamizi Wa Ufuo

23. Majukumu ya bunge
24. Majukumu ya kamati tendaji
25. Mamlaka na wajibu wa mwenyekiti
26. Wajibu wa katibu
27. Wajibu wa mweka hazina

SEHEMU YA VI: Kuhusu fedha na usimamzi wake katika Kundi La Usimamizi Wa Ufuo

*Sehemu*

28. Ufadhili wa Kundi La Usimamizi Wa Ufuo
29. Usimamizi wa fedha na raslimali za Kundi La Usimamizi Wa Ufuo
30. Akaunti za fedha

SEHEMU YA VII**:** KUIMARISHA, KUSAJILIWA, USAIDIZI & UANGALIZI, NA KUTANGULIWA KWA BMU

31. Utaratibu wa kuimarishwa na kusajiliwa katika gazeti la serikali
32. Usajili
33. Usaidizi na uangalizi wa Kundi La Usimamizi Wa Ufuo
34. Kutanguliwa kwa Kundi La Usimamizi Wa Ufuo
SEHEMU YA VIII: MASHARTI YA JUMLA
35. Kizuizi
36. Uharibifu mbaya wa hati za Kundi La Usimamizi Wa Ufuo
37. Adhabu

RATIBA

RATIBA YA KWANZA

RATIBA YA TATU

RATIBA YA NNE

**KANUNI ZA UVUVI (KUNDI LA USIMAMIZI WA UFUO), 2007**

[Toleo la Kwanza]

[L.N. 402/2007.]

SEHEMU YA KWANZA: Utangulizi

1. **Dondoo**

Hizi kanuni zinaweza kunukuliwa kama kanuni za uvuvi (Kundi La Usimamizi Wa Ufuo) 2007

2. **Tafsiri**

Katika kanuni hizi, iwapo hakuna dhana mbadala, "**bunge**" inamaanisha mkutano wa wanachama wa Kundi La Usimamizi Wa Ufuo waliosajiliwa kulingana na maelekezo ya kanuni hizi;

"**Afisa wa uvuvi aliyeidhinishwa**" ni mtu ambaye ako na mamlaka ya usimamizi wa Kundi La Usimamizi Wa Ufuo mwenye cheo cha msaidizi wa afisa wa uvuvi au zaidi yake, aliyeajiriwa katika utumishi wa umma

"**Ufuo**" ina maana ya sehemu maalum ya kijiografia chini ya mamlaka ya Kundi La Usimamizi Wa Ufuo kama ilivyoimarishwa kulingana na kanuni ya 5.

"**Kundi La Usimamizi wa ufuo**" ina maanisha shirika linalo husisha wavuvi, wauzaji samaki, wamiliki maboti, wasindikaji samaki na washika dau wengine ambao wanategemea shughli za uvuvi kupata riziki.

"**Sheria-ndogo**" ina maanisha sheria za usimamizi wa ndani wa Kundi La Usimamizi Wa Ufuo zilizoundwa na bunge na afisa wa uvuvi aliyeidhinishwa.

"**Mwenyekiti**" ina maanisha mwenyekiti wa bunge na Kundi La Usimamizi Wa Ufuo aliyepitishwa na bunge na afisa wa uvuvi aliyeidhinishwa

"**Mpango wa usimamizi usaidizi**" inaamanisha mpango wa kusaidia usimamizi wa sehemu maalum ya uvuvi au jiografia iliyopitishwa kulingana na kanuni nambari 7.

"**Mkurugenzi**" inamaanisha Mkurugenzi wa Uvuvi.

"**Kamati tendaji**" inamaanisha kamati ya wanachama wa Kundi La Usimamizi Wa Ufuo waliochaguliwa kutenda kazi kama ilivyopitishwa na kanuni nambari 14 na 15.

"**Kituo Cha Kutua Samaki**" inaamanisha kituo cha kutua samaki kama ilivyoimarishwa na mkurugenzi kulingana na masharti ya Sheria.

"**Mwanachama**" inamaanisha mwanachama wa Kundi La Usimamizi Wa Ufuo, na

"**Afisa Msimamizi**" inamaanisha Afisa wa Uvuvi aliyeidhinishwa, ama mtu mwingine yeyote aliyemteuwa kwa maandishi kusimamia au kuongoza uchaguzi wa Kundi La Usimamizi Wa Ufuo.

3. **Malengo**

1. Mkurugenzi atawezesha uanzilishaji wa Kundi La Usimamizi Wa Ufuo kwa kila kituo cha kutua samaki

   Kwa sharti kwamba katika kadhia inayofaa, Kundi La Usimamizi Wa Ufuo moja inaweza kuweka kituo cha kutua samaki kimoja au zaidi kulingana na masharti ya usimamizi yaliyotolewa na mkurugenzi.

2. Kundi La Usimamizi Wa Ufuo haitakuwa na misimamo ya kisiasa au kidini.
3. Malengo ya Kundi La Usimamizi Wa Ufuo yatakuwa-
   a) Kuimarisha usimamiaji wa vituo vya kutua samaki, raslimali za uvuvi na mazingira ya majini
   b) Kuisaidia uimarishaji wa maendeleo endelevu ya sekta ya uvuvi
   c) Kusaidia kupunguza umaskini na kuboresha afya, ustawi na maisha ya wanachama kupitia uboreshaji wa mipango na usimamizi wa raslimali, utawala bora, ushiriki katika demokrasia na kujitegemea.
   d) Kutambua mchango wa vitengo tofauti-tofauti katika jamii.
   e) Hakikisha utimizaji wa kiwango cha ubora cha juu kuhusiana na samaki na bidhaa za uvuvi.
   f) Kujenga uwezo wa wanachama kuwezesha usimamiaji bora wa uvuvi kwa kushirikiana na washika dau wengine na,
   g) Kuzuia au kupunguza migogoro katika sekta ya uvuvi.

4. **Muundo wa Utawala**

   Kundi La Usimamizi wa Ufuo litajumuisha-
   a) Bunge
   b) Kamati tendaji, na
   c) Kamati zingine ndogo kulingana na maelezo katika sheria-ndogo za Kundi la Usimamizi wa Ufuo

5. **Eneo la mamlaka la Kundi La Usimamizi wa Ufuo**

   1) Kila Kundi La Usimamizi wa Ufuo litakuwa na mamlaka ya eneo iliyoundiwa kulingana na sheria ya 3
   2) Mkurugenzi, kwa mashauriano na mashirika yanayostahiki na kabla ya kuanzisha Kundi La Usimamizi wa Ufuo, atamudu ukaguaji wa sehemu ambayo kituo cha utuaji samaki kitakuwepo, na mipaka yake kuchorwa na kudhihirishwa.
   3) Kwa minajili ya kuhakikisha usalama wa samaki na bidhaa za uvuvi, sehemu maalum ya Kituo cha Kutua Samaki kitachorwa, kudhihirishwa na kuteuliwa kwa kazi pekee ya kutua na kuuza samaki na bidhaa za uvuvi.
   4) Shughuli ambazo hazihusiani moja kwa moja na kutua au uuzaji wa samaki na bidhaa za samaki ambazo kawaida zimekuwa zikifanyika ufuoni zikiwamo, na sio tu-
      a. Ufuaji wa nguo;
      b. Mifugo kunywa maji;
      c. Uvutaji wa maji kwa matumizi ya nyumbani, na
      d. Utoaji wa huduma kwa ajili ya utalii na burudani,

Zitatengewa sehemu tofauti ufuoni mbali na sehemu iliyo fadhiliwa na aya ya 3 hapa juu.

5) Maelezo ya ufuo, yakiwamo mpango na maelezo ya kijiografia ya sehemu yoyote iliyoteuliwa kwa kazi maalum ya kutua na kuuzia samaki na bidhaa za samaki, itajumuishwa katika sheria-ndogo za kila Kundi la Usimamizi wa Ufuo.
6) Kundi La Usimamizi wa Ufuo lina haki ya kuunda sheria-ndogo zitakazofuatwa na wanachama wake na yeyote ufuoni ama anayetumia ufuo.
7) Kundi La Usimamizi wa Ufuo linaweza kutengeneza sheria-ndogo na amri kuwa shughuli maalum katika ufuo wao zitafanywa na wanachama wake au wanachama wa vikundi vingine vya ufuoni kulingana na ushirikiano kwatika usimamizi unaofaa.
8) Kundi La Usimamizi wa Ufuoni litatekeleza mamalaka yake ufuoni kwa njia ya haki, usawa na bila ubaguzi.
9) Kundi la Usimamizi Ufuoni litaonyesha, katika eneo maarufu-
    a) Tangazo kuwa ufuo unasimamiwa na Kundi la Usimamizi wa Ufuo,
    b) Nakala yake ya sheria-ndogo.

**6. Sheria za maelekezo za Kundi za Usimamizi wa Ufuo.**

1) Kundi simamizi litawajibika kwa wanachama wake na mkurugenzi kuhakikisha usimamizi na matumizi ya kituo cha kutua samaki kwa njia taratibu, salama na ifaavyo, na kwa hili-
    a) Kuhakikisha kuwa kituo cha kutua samaki, pamoja na miundo au majengo yalioko pale, yamewekwa kwa namna ya usafi wa hali ya juu na yenye kuridhisha.
    b) Kuhakikisha usalama wa kituo cha kutua samaki na vyombo vya uvuvi, nyavu au vifaa vingine au majengo ndani ya mipaka yake.
    c) Kuhakikisha viwango vifaavyo vya usafi kuhusu hifadhi ya kituo na hali ya samaki na bidhaa za uvuvi vimefuatwa.
    d) Kuhakikisha usalama na utaratibu katika kituo cha kutua samaki kwa kushirikiana na mashirika mengine, na
    e) Kudumisha, na ikihitajika, kukarabati majengo au miundo katika kituo cha kutua samaki.
2) Kundi la Usimamizi wa Ufuo litakusanya, kuchunguza, kutumia, kuhifadhi na kusambaza taarifa na data yoyote muda kwa muda kama itakavyoelezwa na mkurugenzi kupitia maandishi kuhusiana na kutua na kuuza samaki au bidhaa za uvuvi, ikiwamo, na sio tu-
    a) Idadi ya samaki au bidhaa za uvuvi zilizotua.
    b) Bei ya bidhaa
3) Kundi la Usimamizi wa Ufuo litajitahidi kuhakikisha usalama wa wanachama wake wanaojihusisha na uvuvi, na kwa hili-
    a) Litasimamia na kuhakikisha vyombo viko salama kwendea baharini, na litafanya mikakati kuhakikisha zimefuata kanuni za usalama zikiwamo masharti kuhusiana na matumizi ya vifaa vya usalama binafsi; na
    b) Kufanya mipango ya kutoa vyombo au huduma za kuokoa maisha.
4) Kundi la Usimamizi wa Ufuo litafanya mikakati kuhamasisha wanachama na jamaa zao kuhusiana na hatari za kiafya na juhudi za kupunguza na kuzuia maradhi kama malaria, HIV-AIDS na mengineyo.

5) Kundi la Usimamizi wa Ufuo laweza kutoa mafunzo kwa wanachama wake kuhusu mbinu za uvuvi, soko na usindikaji wa samaki, namna ya kusimamia fedha zao binafsi na mambo mengine muhimu kwa uvuvi, na litasaidia shughuli za vyama vya ushirika na vikundu vya kujitegemea vya uvuvi katika mamlaka yake.
6) Kundi la Usimamizi wa Ufuo lina uhuru wa kudhibiti na kukuza uuzaji wa samaki ikiwamo ujenzi na ugavi wa vifaa vya masoko, na upangaji wa minanda ya samaki, lakini halitakuwa na uhuru, kwa namna yoyote ile, kuamua au kuamuru bei ambayo samaki na bidhaa za uvuvi zitakavyouzwa.
7) Kundi la Usimamizi wa Ufuo linaweza, kupitia idhni ya maandishi kutoka kwa mkurugenzi, kujenga miundo au majengo ambayo ni muhimu ili kutekeleza shughuli zake.
8) Kundi la Usimamizi wa Ufuo linaweza kusaidia kuimarisha hali ya uchumi ya wanachama wake kwa-
    a) Kukuza na kuwezesha uwekezaji katika kituo cha kutua samaki na shughuli za uvuvi ambazo zafanywa hapo.
    b) Kuunga mkono uendelezaji wa mbinu endelevu mbadala za kipato kwa wanachama wake ambazo zina uwezo wa kupunguza uelemeaji wa raslimali za uvuvi zikiwamo, na sio tu, utoaji wa huduma endelevu kwa watalii.
9) Kundi la Usimamizi wa Ufuo linaweza-
    a) Kupanga na kuwezesha ugavi wa vifaa vya uvuvi, barafu au vifaa muhimu kwa wanachama wake; na
    b) Kutoa huduma za akiba na mikopo kwa wanachama wake,

    lakini halina uhuru wa kutoa huduma hizi iwapo tayari zinatolewa na mashirika mengine ufuoni.

**7. Ushirikiano wa usimamizi**

1) Afisa wa Uvuvi aliyeidhinishwa, kwa kufuata mchakato wa mashauriano, kuteuwa kundi la usaidizi kwa kila kundi la Usimamizi wa Ufuo amabalo litakuwa sehemu ambayo litafanya shughuli za usimamizi wa uvuvi kwa kushirikiana na mkurugenzi

2) Katika hali ya uvuvi au maeneo ambayo shughuli za uvuvi zafanywa na wanachama wa zaidi ya kundi moja la usimamizi wa ufuo, afisa wa uvuvi aliyeidhinishwa, kwa kufuata mchakato wa mashauriano, atateuwa eneo moja ambapo makundi zaidi ya moja yanaweza kushirikiana katika majukumu ya usimamizi wa uvuvi pamoja na mkurugenzi.

3) Mkurugenzi, kwa mujibu wa hali iliyoelezwa katika aya ya pili hapa, atateua maeneo ambayo kila kundi la usimamizi wa ufuo litachukua majukumu maalumu hususan katika kushika doria.

4) Kufuatia kuteuliwa kwa eneo la kushirikiana kazi, afisa wa uvuvi aliyeidhinishwa, kwa mashauriano na makundi ya usimamizi wa ufuo, atatengeneza mikakati rasimu ya hili eneo la ushirikiano ambayo itaeleza mikakati ya uvuvi inayofaa kutekelezwa ili kuhakikisha matumizi endelevu ya uvuvi katika eneo hili yakiwamo, na sio tu-
    a) Kuteuliwa kwa sehemu maalum zilizofungwa ambapo shughli zote au maalum za uvuvi zimeharamishwa.

  b) Kuteuliwa kwa nyakati zilizodhibitiwa ima katika kila au baadhi ya sehemu maalum katika eneo la ushirikiano
  c) Kutia alama katika vyombo vya kwendea baharini.
  d) Kuweka masharti kuhusu namna ya nyavu au vifaa vingine vitakvyotumiwa katika uvuvi; na
  e) Kuweka masharti kuhusu idadi ya leseni za vyombo za kuendea baharini au leseni za uvuvi zitakozotolewa.

5) Mipango yote ya ushirikiano yatakuwa ni makubaliano kati ya afisa wa uvuvi aliyeidhinishwa na kundi la usimamizi wa ufuo, na-
  a) Itatekeleza sera na mipango ifaayo ya kitaifa na kikanda.
  b) Kufuata maagizo ya kanuni za uvuvi zilizopo.
  c) Kueleza kazi na majukumu ya vikundi husika za usimamizi wa ufuo na mkurugenzi kuhusiana na utekelezaji wa mipango hii.

6) Afisa wa uvuvi aliyeiidhinishwa atampelekea mkurugenzi mipango ili atoe idhini.

7) Kundi la Usimamizi wa Ufuo litatekeleza makubaliano ya ushirikiano kupitia sheria-ndogo zake.

8) Kundi la Usimamizi wa Ufuo litaunda kamati ndogo ya kushika doria ambalo, kwa kushirikiana na mkurugenzi, litashika doria za kawaida katika eneo la ushirikiano, au katika eneo teule, ili kuhakikisha uzingatiaji wa sheria na sheria-ndogo na mipango yoyote ya ushirikiano.

9) Afisa wa uvuvi aliyeidhinishwa pamoja na kamati tendaji za vikundi vya usimamizi wa ufuo zitasimamia utekelezaji wa mipango ya ushirikiano na kuikagua na kuirekebisha mara kwa mara

10) Ikiwa afisa wa uvuvi aliyeidhinishwa atashuku kuwa kundi la usimamizi wa ufuo halijachukua hatua kutekeleza mipango ya ushirikiano, atashauriana na kundi hili kuhusu sababu zao za kutochukua hatua.

11) Ikiwa ata baada ya mashauriano haya afisa atahisi kwamba kundi lile bado halichukui hatua kutekeleza mipango ya ushirikiano, atatoa maagizo kwa ilani kuonyesha sababu ya kutobatilishwa kwa mipango ile na ikiwa-
  a) Kundi husika la usimamizi wa ufuo litakosa kuonyesha sababu yao kutobatilishwa katika muda wa wa siku 14 baada ya kupokea ilani, au
  b) Afisa wa uvuvi aliyeidhinishwa hajaridhika na majibu ya kundi la usimamzi wa ufuo,

Anaweza kusimamisha au kubatilisha mipango ya ushirikiano, na baada ya kutoa ilani kwa kundi au vikundi husika vya usimamizi wa ufuo kupitia maandhishi atapeleka maamuzi yake kwa mkurugenzi ambaye, katika muda wa siku 14, atapitisha au kuyapinga haya maamuzi.

12) Kundi la usimamzi wa ufuo ambalo limeadhirika na maamuzi ya kusimamisha au kubatilisha mpango wa ushirikiano kulingana na aya ya (11) ya hizi kanuni linaweza, katika muda wa siku 14 za kupata ilani, kukata rufaa kwa mkurugenzi ambaye uamuzi wake ni wa mwisho.

13) Kamati tendaji ya kundi la usimamizi wa ufuo ambalo mpango wa ushirikiano umebatilishwa litasimamishwa na kamati ya muda kuteuliwa kulingana na sharti ya kanuni ya 21.

**8. Ulinzi wa mazingira**

1) Kundi la usimamizi wa ufuo litahakikisha ulinzi wa mazingira ya majini katika eneo lao la ushirikiano na litashirikiana na mamalaka husika katika kutekeleza hili.
2) Kundi la usimamizi wa ufuo lina uhuru wa kujumuisha masharti katika sheria-ndogo zake kuhusiana na ulinzi wa mazingira ya majini katia eneo lake.

**SEHEMU YA TATU: Uanachama na uchaguzi wa** Kundi la Usimamizi wa Ufuo.

**9. Uanachama**

1) Uanachama wa kundi la usimamizi wa ufuo liko wazi kwa watu ambao-
   a) wanategemea shughuli za uvuvi kupata riziki zao kwa njia moja au nyingine katika ufuo ambao uko katika mamlaka ya hilo kundi la usimamizi wa ufuo.
   b) Wako katika moja ya vikundi vya uanachama vilivyoelezwa katika kanuni; na
   c) Wanaweza adhirika vibaya kwa kusitishwa kwa shughuli za uvuvi katika huo ufuo ima kwa muda au kudumu.

2) Kundi la usimamzizi wa ufuo linaweza kuongeza katika sheria-ndogo zake kwamba shughuli maalum katika kituo cha kutua samaki chini ya mamlaka yake zinaweza kufanywa tu na wanachama wake

3) Mtu moja hawezi kwa wakati mmoja kuwa mwanachama wa kundi la usimamizi wa ufuo zaidi ya moja

4) Shirika, kupitia mwakilishi na tangazo lililoandikwa kwa kamati tendaji, linaweza kuwa mwanachama wa kundi la usimamizi wa ufuo

5) Ikiwa chombo cha kuendea baharini kinamilikiwa na watu zaidi ya mmoja, wamiliki watateua mmoja wao kuwa mwanachama wa kundi la usimamizi wa ufuo, na kwa pamoja kuarifu kamati tendaji kuhusu hili.

6) Watu chini ya miaka 18 hawana ruhusa kwa namna yoyote kukubaliwa kuwa wanachama wa kundi la usimamizi wa ufuo wala kupewa jukumu lolote.

**10. Vigawanyo vya uanachama**

1) Kundi la usimamizi wa ufuo litakuwa na vigawanyo vifuatavyo vya wanachama-
   a) Wamiliki maboti, yaani wamiliki wa vyombo vya kuendea baharini vilivyosajiliwa katika ufuo wao;
   b) Wafanyakazi katika vyombo vya kuendea baharini, yaani watu wengine isipokuwa wamiliki maboti ambao leseni zao za uvuvi zinawaidhinisha kuvua kutoka kwa ufuo wao; na
   c) Wachuuzi wa samaki au wagavi vifaa, yaani watu wanaohusika mara kwa mara na uchuuzi wa samaki au ugavi wa vifaa na huduma muhimu kwa uvuvi katika kituo cha kutua samaki.

2) kwa minajili ya hii kanuni, “watu wanaojihusisha katika uchuuzi wa samaki” inajumuisha-
    a) watu wanaojihusisha na kuuza samaki sehemu za karibu kwa uwepo wa leseni zao za kuuza samaki.
    b) Watu wanaojihusisha na kuwauzia samaki watu wengine walioko mbali kwa uwepo wa leseni zao za kuuza samaki.
    c) Watu ambao wanauza vifaa vya kuvulia samaki, chambo, barafu au vifaa vingine kwa wamiliki maboti kwa makubaliano ya kumiliki samaki au bidhaa za uvuvi zitakazotua kwanza kisha kuviuza.
    d) Watu ambao wananunua samaki ufuoni kwa kutengeneza na kuuza ufuoni au katika maeneo ya ufuo kwa uwepo wa leseni ya kuuza samaki.
    e) Wakala au wawakilishi wa watu wanaojihusisha na usindikaji wa samaki kwa kiwango kikubwa kwa uwepo wa leseni ya kuuza samaki, ima wameajiriwa na wasindikaji hawa au la; na
    f) Watu wanaojihusisha, ima kama wafanyakazi au vingine, katika kuainisha, kuchanganua, kuthamini, kufunga na kusafirisha samaki katika huo ufuo.
3) Kwa minajili ya hii kanuni, “watu wanaojihusisha na ugavi wa vifaa na huduma muhimu kwa uvuvi” inajumuisha watengenezaji na wanaokarabati maboti na wanaokarabati nyavu.
4) Katika ile hali uanachama wa mtu katika kundi la usimamizi wa ufuo unategemea mtu yule kuwa na leseni-
    a. Kusimamishwa kwa hii leseni kutaadhiri uanachama wake katika kundi la usimamizi wa ufuo kwa muda sawa.
    b. Kubatilishwa kwa hii leseni pia kutabatilisha uanachama wake katika kundi la usimamizi wa ufuo.

**11. Utaratibu wa kujiunga**

1) Anayetaka kujisajili kama mwanachama wa kundi la usimamizi wa ufuo anapaswa kujisalili kwa kuandikia kamati tendaji.
2) Kamati tendaji itapelekea maombi kwa afisa wa uvuvi aliyeidhinishwa ili kupata idhini yake.
3) Ikiwa afisa wa uvuvi aliyeidhinishwa hapingi maombi haya ndani ya siku 14, na mwenye kujisajili ametimiza masharti yaliyowekwa katika kanuni ya 10, na baada ya kulipa ada itakikanayo atakubaliwa kuwa mwanachama wa kundi la usimamizi wa ufuo na jina lake kuongezwa katika orodha ya wanachama.
4) Ambaye hana leseni itakayomwezesha kuwa mwanachama wa kundi la usimamizi wa ufuo anaweza kuwasilisha ombi la uanachama wa muda.
5) Mwasilishi ombi ana haki ya kupata uanachama wa muda isipokuwa kama-
    a) Hapo awali amewahi kutolewa kutoka kwa kundi hili au linguine la usimamizi wa ufuo.
    b) Mipango ya ushirikiano imeeleza wazi idadi ya leseni haifai kuzidi kiwango fulani na kiwango hiki kimetimia.
    c) Mwasilishaji ombi ana rekodi ya uhalifu.

6) Ikiwa maombi ya uanachama wa muda yaliyowasilishwa yamezidi leseni zilizoko kulingana na mipango ya ushirikiano, maombi yatashughulikiwa kwa njia ya usawa kwa kuwapa kipaumbele masikini na wasiojiweza na wale ambao familia zao zinategemea kipato kutoka kwa eneo la mamlaka la hili kundi la usimamizi wa ufuo.
7) Mkurugenzi hatatoa leseni kwa mtu ambaye anahusika na ufuo fulani isipokuwa kwa ile hali kwamba ni mwanachama wa kawaida au wa muda katika kundi husika la usimamizi wa ufuo.

8) Kufuatia mwanachama wa muda kupata leseni, atapaswa atoe habari kwa kuandikia kamati tendaji ambayo itampa uanachama kwa kujumuisha jina lake katika orodha ya wanachama na pia kumpa kadi na nambari ya usajili wa uanachama.

**12. Kujiuzulu na kutolewa kwenye kundi la Kundi la Usimamizi wa Ufuo.**

1) Mwanachama wa kundi lolote la usimamizi wa ufuo anaweza kujiuzulu wakati wowote kwa kutoa habari kupitia maandishi kwa kamati tendaji, lakini kujiuzulu hakutaadhiri jukumu la mtu yule kulipa ada anazodaiwa.

2) Bunge linaweza fanya maamuzi kumtoa mtu katika uanachama kwa mapendekezo ya kamati tendaji kupitia sababu zifuatazo-
   a. Ameshatakiwa mahakamani kwa kosa linalohusiana na uvuvi
   b. Ameshtakiwa mahakamani na kosa linguine lolote la uhalifu na kuhukumiwa kifungo kinachozidi miezi sita; au
   c. Ameendeleza mienendo inayokanusha malengo ya kundi la usimamizi wa ufuo na sheria-ndogo zake na amepuuza tahadhari tatu zilizoandikwa na kutolewa na kamati tendaji

3) Kutolewa kwa mwanachama kutapitishwa na wengi-rahisi katika kundi la usimamizi wa ufuo kupitia mkutano ulioitishwa na mwenyekiti.

4) Kupitia kutolewa kwa mwanchama, mkurugenzi atasitisha leseni zozote, usajili au kibali kinachohusiana na ufuo huo.

5) Aliyetolewa kutoka kwa kundi la usimamizi wa ufuo hataruhusiwa kujiunga tena kama mwanachama kwa muda wa miaka miwili tangia tarehe ya kutolewa.

6) Ambaye hajaridhia kutolewa kutoka kwa kundi la usimamizi wa ufuo anaweza kukata rufaa kwa kuandikia mkurugenzi chini ya muda wa siku 14 tangia tarehe ya kutolewa na uamuzi wa mkurugenzi utakuwa ndio wa mwisho.

**13. Haki na majukumu ya wanachama wa Kundi la Usimamizi wa Ufuo**

1) Mwanachama wa kundi la usimamizi wa ufuo anaweza-
   a) Kushiriki katika mchakato wa maamuzi katika kundi la usimamizi wa ufuo
   b) Kusimama ili kuchaguliwa na kushiriki katika uchaguzi iwapo hana deni kuhusina na ada au malipo katika kundi la usimamizi wa ufuo.
   c) Kufaidika kwa huduma zozote zinazotolewa na kundi la usimamizi wa ufuo kwa wanachama wake ikiwa amelipa ada au malipo yanayotakikana; na
   d) Kukagua vitabu na kumbukumbu zinazotakiwa kuhifadhiwa na kundi la usimamizi wa ufuo.

2) Mwanachama wa kundi la usimamizi wa ufuo anaweza-
   a) Kufuata sheria-ndogo
   b) Kufuata masharti ya Sheria za Uvuvi (Cap. 378.).
   c) Kuhakikisha leseni alizopewa kulingana na Sheria za Uvuvi zimesasishwa.
   d) Kufuata maagizo ya kisheria kutoka kwa afisa wa uvuvi aliyeidhinishwa au afisa rasmi wa kundi la usimamizi wa ufuo.
   e) Kulipa bila kuchelwa ada au malipo yanayodaiwa na kundi la usimamizi wa ufuo.
   f) Kutoharibu mali inayomilikiwa na kundi la usimamizi wa ufuo.
   g) Kutoa taarifa kwa kundi la usimamizi wa ufuo kuhusu kutua na kuuza samaki kama itakavyotakiwa

**14. Kamati Tendaji**

1) Kamati tendaji ya kundi la usimamizi wa ufuo yatakiwa kuwa na wanachama wasiopungua 9 wala kuzidi 15 kama inavyotakiwa katika sheria-ndogo zake, ambao watachaguliwa na kundi la usimamizi wa ufuo.

2) Muundo wa kamati tendaji utaelezwa katika sheria-ndogo za kila kundi la usimamizi wa ufuo kwa matakwa-
    a) Kuwa uanachama utagawanywa kama ifuatavyo-
        i. Wamiliki maboti- 30%
        ii. Wafanyakazi katika vyombo vya kuendea baharini- 30%
        iii. Wachuuzi- 10%
        iv. Wengine- 30%
    b) Kando na matakwa ya aya (a), kwa vyovyote vile, kamati tendaji iwe na wanawake angalau watatu.

3) Kila mwanachama wa kamati tendaji atakuwa na jukumu, katika utendaji kazi wake, la kuwakilisha maslahi ya kundi nzima la usimamizi wa ufuo wala sio tu maslahi ya uanachama maalum ambao yeye yumo.

4) Kamati tendaji itakuwa na mwenyekiti, makamu mwenyekiti, katibu, mweka hazina na wanakamati.

**15. Kuchaguliwa kujiunga na kamati tendaji**

1) Mwanachama wa kundi la usimamizi wa ufuo anaweza kuteuliwa kuchaguliwa katika kamati tendaji ikiwa-
    a) Ni raia wa Kenya na ako na kitambulisho au paspoti au leseni ya kuendesha gari;
    b) Isipokuwa wagomeba katika uchaguzi unaofanyika wakati wa kuunda kundi la usimamizi wa ufuo, awe ashakuwa mwanachama wa kundi la usimamizi wa ufuo kwa muda wa zaidi yam waka mmoja.
    c) Ana akili timamu.
    d) Hana rekodi ya uhalifu.
    e) Hajapatikana na kosa la kukiuka sheria-ndogo za kundi la usimamizi wa ufuo.
    f) Hadaiwi ada au malipo na kundi la usimamizi wa ufuo.
    g) Ugombea wake uwe umepitishwa na wanachama wengine kumi wa kundi la usimamizi wa ufuo ambao watakuwa katika kigawanyo kimoja cha uanachama katika FORM FD/NF/1 kulingana na maagizo ya Ratiba Ya Tatu katika kanuni hizi;
    h) Ana uwezo wa kusoma na kuandika, isipokuwa katibu na mweka hazina ambao watatakiwa kuwa na cheti cha shule ya msingi

2) Afisa msimamizi atatangaza mwanzo wa kipindi cha kampeni kisichozidi siku saba kabla ya siku ya uchaguzi.

3) Kundi la usimamizi wa ufuo litaeleza katika sheria-ndogo zake ikiwa-
    a) wagombea watasimama moja kwa moja kuchaguliwa kwa nafasi za mwenyekiti, makamu mwenyekiti, katibu na mweka hazina, au
    b) watasimama kuchaguliwa kwenye kamati tendaji na uchaguzi kwa nafasi hizi kufanywa na kutoka kwenye wanachama wa kamati tendaji.

4) Uchaguzi kwa kamati tendaji utakuwa kupitia kura ya siri.

5) Baada ya kuhesabu na kutangaza matokeo ya uchaguzi, afisa msimamizi atawasilisha matokeo kwa mkurugenzi kwa FORM FD/ER kulingana na maagizo katika Ratiba Ya Nne ya kanuni hizi.
6) Mwanachama wa kamati tendaji-
    a) Atakaa ofisini kwa muda wa mwaka mmoja zaidi;
    b) Anaweza kusimama kuchaguliwa kwa muhula wa miaka minne tena;
    c) Hatasimama kuchaguliwa tena baada ya kumalizika muhula wa pili, lakini anaweza simama kuchaguliwa tena baada ya miaka minne kutoka ofisini.

**16. Kuundwa na kuchaguliwa kijiunga na kamati ndogo**

1) Kundi la usimamizi wa ufuo, kupitia sheria-ndogo zake, litawezesha uundaji wa kamati ndogo kulingana na mahitaji yake maalum

2) Wanachama wa kawaida wa kamati tendaji wtachaguliwa na kamati tendaji kuongoza kamati ndogo zilizoundwa.

3) Bunge, kupitia muundo wa upigaji kura ulioamuliwa na afisa wa uvuvi aliyeidhinishwa, litachagua wanachama kutumikia kamati ndogo.

4) Mwenyekiti wa kamati tendaji, kwa heshima, atakuwa mwanachama katika kamati zote ndogo.

## SEHEMU YA IV: Usimamizi wa Kundi la Usimamizi wa Ufuo

**17. Mikutano ya wanachama wa Kundi la Usimamizi wa Ufuo**

1) Mkutano wa wanachama wa kundi la usimamizi wa ufuo ulioitishwa kulingana na masharti ya kanuni hizi itajumuisha bunge la kundi la usimamizi wa ufuo.

2) Mkutano huu utafanyika angalau mara moja baada ya miezi mitatu, katika mkutano mkuu wa mwaka au mara kwa mara kama ilivyopitishwa katika sheria-ndogo

3) Mikutano zaidi ya wanachama wa kundi la usimamizi wa ufuo yanawezaitishwa na kamati tendaji inapotakikana na itaitishwa baada ya ombi lililoandikwa na ushuru wa wanachama wa kundi la usimamizi wa ufuo.

4) Sheria-ndogo zitaeleza ikiwa kufanya maamuzi katika bunge kutafanyika kwa-
    a) Kunyanyua mikono;
    b) Kunyanyua mikono, isipokuwa katika uchaguzi wa kura ya siri;
    c) Kunyanyua mikono, au kwa kura ya siri kwa hali maalum kulingana na maamuzi ya bunge; au
    d) Kura ya siri.

5) Kila mhusika katika bunge atapswa kupiga kura.

6) Isipokuwa kwa hali ambayo imeelezwa katika hizi kanuni, pendekezo kwa bunge. litachukuliwa kuwa limekubalika ikiwa litapitishwa na zaidi ya nusuya watu walioko.

7) Idadi itakayohitajika kufanya mkutano wa bunge itakuwa ni nusu ya wanachama

8) Mkutano wa bunge ambao idadi hii haijatimia utaairishwa kwa muda usiozidi siku kumi.

9) Mkutano utaongozwa na mwenyekiti wa kamati tendaji au kama hayupo, makamu mwenyekiti.

10) Kwa uamuzi wa mwenyekiti, watu amabao sio wanachama wa kundi la usimamizi wa ufuo au ni wanachama wa kundi la usimamizi wa ufuo lakini hawana idhini ya kupiga kura katika mikutano wanaweza karibishwa kuzungumza bungeni.

11) Afisa wa uvuvi aliyeidhinishwa au yeyote aliyeteuliwa naye atakuwa na idhini ya kuhudhuria mkutano.

**18. Kongamano la bunge**

1) Kamati tendaji, ndani ya siku 30 kabla ya kuita mkutano wa bunge, itabandika tangazo katika sehemu maarufu ufuoni, katika ofisi za kundi la usimamizi wa ufuo na sehemu zingine za umma katika eneo ili kuwezesha wanachama wa kundi la usimamizi wa ufuo kujua kuhusu mkutano uliopangwa.

2) Tangazo kama hili lilioelezwa katika aya ya (1) litaashiria tarehe, wakati na mahali pa mkutano wa bunge, na rasimu ya ajenda ya bunge.

**19. Mikutano ya kamati tendaji**

1) Kamati tendaji itakutana angalau mara moja kwa mwezi.

2) Idadi itakayohitajika kufanya mkutano wa bunge itakuwa ni nusu ya wanachama

3) Maamuzi ya kamati tendaji yatafanywa kwa makubaliano, la sivyo kura itafanywa kwa kila mwanachama kuwa na kura moja

4) Mikutano zaidi ya kamati tendaji inawezaitishwa na mwenyekiti ikitakikana na itaitishwa kwa ombi la thuluthi ya wanachama wake.

5) Afisa wa uvuvi aliyeidhinishwa au mtu aliyeteuliwa kupitia maandishi kwa niaba yake atakuwa na haki yakuhudhuria mikutano ya kamati tendaji kama mwangalizi.

**20. Kuachishwa uanachama wa kamati tendaji na bunge**

1) Bunge linaweza kuondoa mwanachama wa kamati tendaji, au wa kamati zozote ndogo kwa sababu zifuatazo-

a) Kuna Ushahidi kuwa hana akili timamu
b) Amekosa kuhudhuria mikutano mitatu kufuatana bila sababu ya kueleweka.
c) Amejihusisha au kukubaliana na shughli bandia za uvuvi.
d) Amekosa kutekeleza majukumu yake kama yalivyoelezwa katika kanuni hizi au katika sheria-ndogo, au
e) amehukumiwa kwa kosa la kihalifu.

2) Bunge kukubali kutolewa kwa mwanachama yeyote wa kamati tendaji litapitishwa kupitia ombi kwa maandishi na thuluthi ya wanachama wa kundi la usimamizi wa ufuo, kwa kueleza sababu za kutolewa.

3) Uamauzi wa kumtoa mwanachama wa kamati tendaji itafanywa kwa kura ya siri inayohitaji wengi-rahisi kwa mapendekezo ya kutolewa, na kudhibitishwa kwa kuandikwa na afisa wa uvuvi aliyeidhinishwa.

4) Mwanachama wa kamati tendaji aliyetolewa kulingana na kipande cha (1) cha hizi kanuni anaweza kukata rufaa ndani ya siku 14 kwa kumuandikia mkurugenzi na kueleza msingi wa rufaa.

5) Mkurugenzi ataamua kuhusu rufaa ndani ya siku 14 baada ya kupokea ombi, na atatoa habari kwa kundi la usimamizi wa ufuo na afisa wa uvuvi aliyeidhinishwa.
Ikiwa thuluthi mbili au zaidi ya kamati tendaji imetolewa kwenya kamati, basi kamati tendaji nzima itatolewa na afisa wa uvuvi aliyeidhinishwa atateuwa kamati ya muda na kuitisha uchaguzi upya ndani ya siku 90 za kutolewa

**21. Kusimamishwa kwa kamati tendaji na mkurugenzi.**

1) Mkurugenzi au afisa wa uvuvi aliyeidhinishwa, kwa sababu kuwa kamati tendaji au wanakamati wake wamejihusisha au kukubaliana na shughuli za uvuvi zilizopigwa marufuku, watasimamisha kamati au wanakamati na kuteuwa kamati au wanakamati wa muda.

2) Wakati afisa wa uvuvi aliyeidhinishwa atafanya uamuzi kama huu, na sio mkurugenzi, afisa atatoa taarifa kuhusu hii kesi kwa kuandika sababu za uamuzi huu kwa mkurugenzi.

3) Kamati au mwanakamati yeyote aliyekerwa na uamuzi wa afisa wa uvuvi aliyeidhinishwa anaweza, ndani ya muda wa siku 14 baada ya kupata taarifa hii, kukata rufaa kwa mkurugenzi.

4) Mkurugenzi anaweza kuunga mkono, kutofautiana au kubadili uamuzi na vile vile kutoa maagizo kwa afisa wa uvuvi aliyeidhinishwa.

5) Uamuzi wa mkurugenzi katika aya ya (4) utakuwa ni wa mwisho.

6) Ikiwa mkurugenzi ataamua kusimamisha kamati, basi afisa wa uvuvi aliyeidhinishwa ataataitisha uchaguzi upya kubadilisha kamati au wanakamati waliotolewa ndani ya siku tisaini ya uamuzi wa mkurugenzi.

7) Kamati tendaji au mwanakamati aliyetolewa atarudisha kadi ya mamlaka kwa afisa mtoaji kulingana na hizi kanuni

**22. Waajiriwa wa Kundi la Usimamizi wa Ufuo**

1) Kundi la usimamizi wa ufuo linaweza kuajiri wafanyakazi wa muda mchache au muda mrefu kama inavyohitaji kulingana na bajeti iliyopitishwa, na sio tu, meneja, mhasibu, baharia, walinzi na wasafishaji.

2) Mwajiriwa wa kundi la usimamizi wa ufuo hana haki ya kugombea katika uchaguzi.

## SEHEMU YA V: Majukumu ya vikundi maalum na maafisaa wa BMU

### 23. Majukumu ya bunge

1) Majukumu ya bunge la kundi la usimamizi wa ufuo ni-

a) kupitisha mipango yoyote ya usimamizi wa ufuo
b) kupitisha rasimu za ushirikiano katika usimamizi
c) kupitisha vitambulisho rasimu na mpango-kazi wa kundi la usimamizi wa ufuo.
d) kupitisha ripoti za mwaka na akaunti za kundi la usimamizi wa ufuo.
e) kupitisha kiwango cha ada na malipo yatakayotozwa wanachama wa kundi la usimamizi wa ufuo.
f) kupitisha sheria-ndogo mpya na kurekebisha zilizoko.
g) Kuchagua wanachama wa kamati yoyote.
h) Ikihitajika, kutoa ofisini wanachama wa kamati tendaji, na
i) Kufanya shughuli zozote ambazo zimeelezwa katika kanuni hizi au sheria-ndogo

2) Bunge la kundi usimamizi wa ufuo halina uhuru wa kutafuta, kwa njia moja au nyingine, kuingilia kati, kupanga upya au kubadilisha uhusiano wa kiuchumi kati ya wanachama walioko katika vigawanyo tofauti za uanachama.

3) Kuhusiana na kupitishwa na kurekebisha sheria-ndogo-

a) Marekebisho yoyote kwa sheria-ndogo zilizopitishwa wakati wa kuunda kundi la usimamizi wa ufuo zitafanyiwa kazi tu kwa idhini iliyoandikwa na mkurugenzi.

b) Nakala ya sheria-ndogo zilizoongezwa au marekebisho yoyote hapo, zapaswa zipelekwe kwa mkurugenzi ndani ya siku 14 kupata idhini yake.

c) Ikiwa mkurugenzi hatatoa jawabu baada ya siku 21 tangia kupokea hizi nakala basi hizi nakala zitachukuliwa kwamba zimeidhinishwa.

d) Mkurugenzi anaweza, ndani ya muda wa siku 21, kutoa habari kwa maandishi kwa kundi husika la usimamizi wa ufuo kwamba hajakubaliana na sheria-ndogo au marekebisho, na kueleza sababu za uamuzi wake na kwa hali hii zitasimamishwa.

4) mkurugenzi anaweza kukataa kupitisha sheria-ndogo au marekebisho kwa sababu zifuatazo-

a) Hazizingatii Sheria Za Uvuvi (Cap. 378), kanuni hizi au kanuni zingine zilizoko
b) Kwa maoni yake, yanazuia malengo ya kundi la usimamizi wa ufuo

5) Ndani ya siku 14 baada ya kupokea tangazo kulingana na aya (4)(d), ya kanuni hizi, kundi la usimamizi wa ufuo linaweza kukataa rufaa kwa maandishi kwa Waziri, ambaye uamuzi wake ni wa mwisho.

### 24. Majukumu ya kamati tendaji

1) Majukumu ya kamati tendaji ni-

a) Kusimamia usimamizi kwa jumla wa shughuli za kundi la usimamizi wa ufuo na kutekelezwa kwa sheria-ndogo zake
b) Kupitisha kumbukumbu za mikutano iliyopita.
c) Kusimamia na kupitia utekelezaji wa mipango ya ushirikiano.
d) Kuwakilisha kundi la usimamizi wa ufuo katika mahusiano yake na makundi mengine
e) Kuita na kutayarisha bunge, ikiwamo kutayarisha ajenda.
f) Kupitia maombi ya kujiunga na kundi la usimamizi wa ufuo, kujiuzulu kutoka kundi na kufanya mapendekezo kwa bunge kuhusu kutolwea kwa wanachama.
g) kuwasilisha rasimu ya mipango ya ushirikiano na kanuni zingine bungeni
h) Kuwasilisha bajeti rasimu bungeni.
i) Kukamilisha mikataba kulingana na mipango na bajeti iliyopitishwa.
j) Kuajiri na kuachisha kazi wafanyakazi wa kundi la usimamizi wa ufuo.
k) Kuhifadhi hisabu na madaftari kulingana na maagizo ya hizi kanuni.
l) Kubadilishana habari na vikundi vingine vya usimamizi wa ufuo kuhusu haki na uwazi katika kuweka bei ya samaki na bidhaa za uvuvi.
m) Kutengeneza mapendekezo ya kutafuta ufadhili, kutayarisha ripoti za fedha na kuwasilisha katika bunge kwa kuidhinishwa.
n) Kukagua na kusajili vyombo vya baharini vya kigeni na kuwapa ruhusa kutua mahali panapofaa.
o) Kusimamia usimamizi wa fedha za kundi la usimamizi wa ufuo.
p) Kuhakikisha maboti ya kuvua samaki katika eneo lao la mamlaka yana vibali vya usalama wa kuendea baharini na zimewekwa vifaa vya kuokoa maisha, na
q) Kufanya shughuli zingine kama zinavyoelezwa katika kanuni hizi au sheria-ndogo

**25. Mamlaka na wajibu wa mwenyekiti**

1) Mwenyekiti wa kundi la usimamizi wa ufuo ata-
a) Ongoza bunge na mikutano ya kamati tendaji.
b) Kuwa msemaji rasmi wa vikundi vingine chini ya kundi la usimamizi wa ufuo.
c) Hakikisha uwasilishaji kwa wakati wa data, habari na ripoti za fedha kutoka kwa kamati kupelekwa kwa bunge na mkurugenzi.
d) Kwa madhumuni ya kutekeleza Sheria na kanuni zozote zilizoundwa, kuwa na nguvu ya kumkamata yeyote anayeamini ametenda uhalifu.
e) Zuia samaki, vyombo vya kuvulia samaki, vyombo vya kuendea baharini au vifaa vingine anaamini vimetumika kutenda uhalifu, ama kuwa sababu ya uhalifu kutendeka.
f) Wasilisha kwa afisa wa uvuvi aliyeidhinishwa haraka iwezekanavyo, yeyote aliyekamatwa au vyombo vilivyozuiwa kulingana na masharti ya kanuni hizi; na
g) Kufanya shughuli zingine kama ilivyoelezwa katika kanuni hizi au sheria-ndogo.

2) Bila ya ubaguzi wa masharti katika kanuni hizi, nguvu za mwenyekiti zitakuwa katika eneo lake la mamlaka kulingana na uongozi wa mkurugenzi.

**26. Wajibu wa katibu**

1) Katibu wa kundi la usimamizi wa ufuo ata-
a) itisha mikutano ya kamati tendaji kwa mashauriano na mwenyekiti.

b) kuwa kiranja wa kuchukua kumbukumbu katika bunge na kwa mikutano ya kamati tendaji.
c) dumisha mwasiliano katika kundi la usimamizi wa ufuo.
d) kusanya ripoti za utendakazi za mwezi, kila robo mwaka na kila mwaka ili kuwasilisha kwa kamati tendaji.
e) hifadhi na kusasisha rekodi zote za wanachama wa kundi la usimamizi wa ufuo na pia vifaa, takwimu na rekodi zingine.
f) kusanya na kuwasilisha data na habari zote kulingana na mahitaji ya mkuirugenzi, na
g) fanya kazi zingine kwa maagizo ya mwenyekiti.

**27. Wajibu wa mweka hazina**

Mweka hazina wa kundi la usimamizi wa ufuo ata-

a. tayarisha na kufanya malipo yaliyopitishwa na kamati tendaji.
b. hifadhi rekodi za shughuli za kifedha zinazofanywa na kundi la usimamizi wa ufuo.
c. kupokea na kuweka pesa katika akaunti ya benki ya kundi la usimamizi wa ufuo.
d. hifadhi kumbukumbu za raslimali na dhima za kundi la usimamizi wa ufuo.
e. tayarisha rekodi za fedha za kila mwezi, kila robo mwaka na kila mwaka.
f. wasilisha ripoti za fedha kwa kamati tendaji na bunge kwa uchunguzi na kupitishwa, na
g. fanya shughuli nyingine kwa maagizo ya mwenyekiti.

**SEHEMU YA VI: Kuhusu fedha na usimamzi wake katika Kundi la Usimamizi wa Ufuo**

*Sehemu*

**28. Ufadhili wa Kundi la Usimamizi wa Ufuo**

1) Kundi la usimamizi wa ufuo linaweza, kwa kupitishwa na mkurugenzi kwa maandishi, weka ada na malipo kwa wanachama wake na watumiaji wengine wa ufuo kulingana na huduma linalotoa kuhusiana na uendeshaji na usimamizi wa ufuo na kujihusisha kwake katika shughuli za ushirikiano kulingana na kanuni ya 7.

2) Ada na malipo yanayokusudiwa katika kipengele cha kanuni (1) ni kama-

a) Ada zinazopaswa kulipwa na kila mwanchama.
b) Ada za usajili za kila mwaka kwa vyombo vya kuvulia samaki.
c) Ada ya kujiunga ya wanachama wapya.
d) Ada za kutua zinazotozwa vyombo vya kuvulia samaki au bidhaa za samaki katika kituo cha kutua samaki.
e) Malipo kwa ajili ya utumizi wa vifaa au huduma zinazotolewa na kundi la usimamizi wa ufuo.
f) Malipo ya kodi kuhusiana na nyumba au majengo yaliyoko katika kituo cha kutua samaki.
g) Ada ya wachuuzi wanaohusika na uuzaji wa samaki

3) Vyanzo vingine vya kipato kwa kundi la usimamizi wa ufuo ni kama ufadhili au michango kutoka kwa serikali, watu binafsi, mashirika yasiyo ya kiserikali au mashirika mengine ya kutoa ufadhili.

**29. Usimamizi wa fedha na raslimali za Kundi la Usimamizi wa Ufuo.**

1) Kuhusiana na usimamizi wa fedha na raslimali zake, kundi la usimamizi wa ufuo lita-

a) Fungua akaunti moja au zaidi katika benki, na wenye kutia saini watakuwa mwenyekiti na mweka hazina na watu wengine watakaochaguliwa na kamati tendaji kupitia maandishi.
b) Anzisha hifadhi ya akiba ili kusimamia gharama zisizopangiwa, na
c) Kwa muongozo wa mkurugenzi, kuanzisha muundo mzuri wa usimamizi wa fedha ili kusaidia katika shughuli zao za kifedha.

2) Kundi la usimamizi wa bahari litahifadhi kumbukumbu na rekodi zifuatazo-

a) Sajili ya wanachama, itakayokaguliwa na kusaishwa baada ya kila miezi mitatu, na itajumuisha jina, anwani na kigawanyo cha uanachama cha kila mwanachama.
b) Sajili ya vyombo na vifaa vinavyomilikiwa na wanachama wa kundi la usimamizi wa ufuo
c) Rekodi inayojumuisha kumbukumbu za mikutano ya bunge
d) Rekodi inayojumuisha kumbukumbu za mikutano ya kamati tendaji.
e) Rekodi za shughuli za kifedha na mikataba.
f) Hesabu ya raslimali zinazomilikiwa na kutumiwa na kundi la usimamizi wa ufuo, na
g) Akaunti za fedha kulingana na kanuni ya 30.

**30. Akaunti za fedha**

1) Kundi la usimamizi wa ufuo litahifadhi kumbukumbu zote za risiti na matumizi na litatengeneza mizania ya kila mwaka na maelezo ya mapato na matumizi kwa muundo uliobainishwa na mkurugenzi.

2) Bunge, kwa mapendekezo ya kamati tendaji itapitisha kila mwaka mizania na maelezo ya mapato na matumizi.

3) Ndani ya muda wa siku 120 baada ya kutimia mwaka wao wa fedha, kamati tendaji ya kila kundi la usimamizi wa ufuo itatayarisha ripoti ya kuonyehsa matumizi ya fedha ya mwaka na kuwasilisha kwa mkurugenzi, kwa muundo uliobainishwa pamoja nan akala ya mizania na maelezo ya mapato na matumizi pamoja na ada ya kuwasilisha iliyobainishwa.

**SEHEMU YA VII: KUIMARISHA, KUSAJILIWA, USAIDIZI & UANGALIZI, NA KUTANGULIWA KWA KUNDI LA USIMAMIZI WA UFUO.**

**31. Utaratibu wa kuimarishwa na kusajiliwa katika gazeti la serikali**

1) Kundi la watu ambalo limenuia kusajiliwa na kupitishwa kama kundi la usimamizi wa ufuo litawasilisha ombi la kuanzishwa kwa kundi la usimamizi wa ufuo kwa mkurugenzi katika FORM FD/A5 kulingana na Ratiba Ya Kwanza katika kanuni hizi, na kwa sharti kuwa katika wanachama wengine, imetiwa saini na angalau wamiliki maboti 30.

2) Kufuatia utafiti na ufafanuzi wa ufuo kulingana na kanuni ya 5(2) ya hizi kanuni, afisa wa uvuvi aliyeidhinishwa atawezesha kuwekwa kwa tangazo katika sehemu maarufu ufuoni kutangazia wanaotaka kuwa wanachama wa kundi la usimamizi wa ufuo kujisajili kuwa wanachama ndani ya siku 30.

3) Kufuatia kumalizika kwa kuda huu wa siku 30, afisa wa uvuvi aliyeidhinishwa atawezesha kuwekwa kwa tangazo ufuoni ya orodha ya watu wanaotarajia kuwa wanachama na ataalika maoni kuhusu orodha hii.

4) Kulingana na maoni yatakayopokewa, afisa wa uvuvi aliyeidhinishwa atakamilisha orodha ya wanachama watarajiwa.

5) Afisa wa uvuvi aliyeidhinishwa ataita mkutano na wanachama watarajiwa kutoka vigawanyo vyote vya uanachama kuchagua wawakilisha wa muda baina ya watano na kumi.

6) Afisa wa uvuvi aliyeidhinishwa atafanya kazi na wawakilisha wa muda kuamua na kurasimu sheria-ndogo za kundi la usimamizi wa ufuo.

7) Kufuatia utayarishaji wa sheria-ndogo rasimu iliyokubaliwa atapanga mkutano ambapo wanachama watarajiwa watajadili na kupitisha sheria-ndogo rasimu.

8) Kufuatia kukamilika kwa mkutano, afisa wa uvuvi aliyeidhinishwa atawasilisha hati zifuatazo kwa mkurugenzi-
   a. Kumbukumbu za mkutano wa wanachama watarajiwa.
   b. Sheria-ndogo rasimu zilizopitishwa.
   c. Ombi la kuanzishwa kwa kundi la usimamizi wa ufuo katika FORM FDIAS kulingana na Ratiba Ya Kwanza ya hizi kanuni.

9) Mkurugenzi atatathmini hati zilizowasilishwa kwake kulingana na aya ya (8) na anaweza-
   a. Kupitisha ombi ikiwa ameridhika nalo na hati zilizoambatanishwa ziko sawa.
   b. Kurejesha ombi na hati zilizoambatanishwa kwa afisa wa uvuvi aliyeidhinishwa na kuandika sababu zake ikiwa hajaridhishwa.

10) Yeyote ambaye hajaridhishwa na uamuzi wa mkurugenzi, kwa kufuata aya ya (9) anaweza kukata rufaa kwa Waziri kulingana na masharti ya kanuni ya 34 ya Kanuni (jumla) za Uvuvi.

11) Baada ya kupitisha ombi, mkurugenzi, kupitia tangazo katika Gazeti la Taifa, ataanzisha kundi la usimamizi wa ufuo na kutoa cheti cha usajili (FORM FD/CR3) kama ilivyoelezwa katika Ratiba Ya Pili katika kanuni hizi

**32. Usajili**

1) Mkurugenzi ataanzisha na kuhifadhi sajili ya vikundi vya usimamizi wa ufuo ambayo itajumuisha maelezo yafuatayo ya kila kundi lausimamizi wa ufuo-
   a. Jina
   b. Ofisi kuu
   c. Idadi ya wanachama

   d. Majina, anwani na nambari za simu za mwenyekiti na wanachama wa kamati tendaji; na
   e. Tarehe ya kuwasilishwa kwa ripoti ya matumizi ya fedha ya karibuni pamoja na nakala ya hio ripoti.

2) Sajili ya vikundi vya usimamizi wa ufuo itakuwa wazi kukaguliwa na umma wakati wa masaa ya kawaida ofisini.

**33. Usaidizi na uangalizi wa Kundi La Usimamizi wa Ufuo.**

1) Mkurugenzi atawajibika kusaidia uanzilishaji na uendeshaji wa vikundi vya usimamizi wa ufuo na kusimamia utendakazi wao wa kiufundi, kisheria na kifedha.

2) Afisa wa uvuvi aliyeidhinishwa kwa ajili ya kundi la usimamizi wa ufuo-
   a. Kuwa afisa msimamizi katika uchaguzi wake
   b. Kuhudhuria mikutano ya wanachama mara kwa mara
   c. Kuwezesha utoaji wa usaidizi wa kiufundi na vinginevyo.
   d. Kutoa uongozi na usaidizi kwa jumla; na
   e. Kufanya shughuli zingine kama inavyoelezwa katika hizi kanuni.

3) Afisa wa uvuvi aliyeidhinishwa atawezesha ukaguzi wa kila mwaka wa akaunti za fedha za kundi la usimamizi wa ufuo na mtu ambaye amehitimu kwa ruhusa ya mkurugenzi mteule.

4) Afisa wa uvuvi aliyeidhinishwamara kwa mara anaweza kuitisha kutoka kwa kundi la usimamizi wa ufuo-
   a. Nakala za akaunti pamoja na nakala za hati na rekodi zinazofaa kuhifadhiwa kulingana na hizi kanuni.
   b. Habari kuhusu utendakazi wao.
   c. Habari na nyaraka kuhusiana na utekelezaji wa mipango ya ushirikiano; na
   d. Habari nyingine atakazohitajia kuridhika kuwa kundi la usimamizi wa ufuo linaendeshwa kisheria.

5) Afisa wa uvuvi aliyeidhinishwa anweza kuulizia kuhusu mwenendo wa shughuli za kundi la usimamizi wa ufuo na kukagua hati na rekodi zake, na kuhoji wanachama wake-
   a. Kwa mujibu wa Ushahidi dhabiti wa wanachama watatu au zaidi ambao wameshtakia mwenendo mbovu, au
   b. Ikiwa, baada ya kukagua nakala za ripoti ya kila mwaka ya fedha na akaunti za hilo kundi la usimamizi wa ufuo, maoni ya mkurugenzi uwepo wa ushahidi usio na shaka kuhusu uvujaji wa fedha na makosa mengine.

6) Ikiwa baada ya ukaguzi au uchunguzi zaidi afisa wa uvuvi aliyeidhinishwa atapata Ushahidi usio na shaka kuhusu uvujaji wa fedha, mwenendo muovu au kwamba kundi la usimamizi wa ufuo halijakuwa likiendeshwa kulingana na masharti ya hizi kanuni, atahitaji kuagiza kamati tendaji ifanye mkutano wa bunge ili awasilishe matokeo ya uchunguzi kwa wanachama wa kundi la usimamizi wa ufuo.
7) Ikiwa kamati tendaji itakosa kuita mkutano wa bunge ndani ya siku 30, afisa wa uvuvi aliyeidhinishwa anaweza kusimamisha kamati yake na aitishe mkutano

kama ule yeye mwenyewe na kuarifu mkurugenzi kuhusu uamuzi wa kusimaisha kamati.

8) Ikiwa kamati tendaji imesimamishwa au kutolewa kulingana na iliovyoelezwa katika aya iliotangulia, afisa wa uvuvi aliyeidhinishwa anaweza kumteua meneja kuendesha kundi la usimamizi wa ufuo mpaka wakati uchaguzi upya utakapofanyika.

9) Mwanachama wa kamati tendaji ambaye hajaridhika nan a uamuzi huu wa afisa wa uvivu aliyeidhinishwa anapswa, chini ya siku 14, kukata rufaa kwa kumuandikia mkurugenzi ambaye uamuzi wake utakuwa wa mwisho.

10) Ikiwa mkurugenzi atapitisha uamuzi wa afisa wa uvuvi aliyeidhinishwa, ataitisha uchaguzi upya kubadilisha kamati au wanakamati waliotolewa chini ya siku tisaini ya uamuzi wa mkurugenzi.

**34. Kutanguliwa kwa Kundi la Usimamizi wa Ufuo**

1) Waziri, kupitia tangazo litakalochapishwa katika Gazeti la Taifa, atatangua kundi la usimamizi wa ufuo kwa moja au zaidi ya hizi sababu-
   a. Kazi ya kundi la usimamizi wa ufuo imeisha
   b. Kundi la usimamizi wa ufuo haliwezi tena kutekeleza kazi yake.
   c. Kundi la usimamizi wa ufuo limefilisi.
   d. Wanachama wa kundi la usimamizi wa ufuo wamejihusisha mara nyingi na uhalifu; au
   e. Uwepo wa kundi la usimamizi wa ufuo hauhitajiki tena.

2) Kufuatia uchapishaji wa uamuzi kuhusu kutanguliwa kwa kundi la usimamizi wa ufuo, Waziri atateua mtu wa kumaliza deni la kundi la usimamizi wa ufuo ili kuhitimisha mambo yake.

## SEHEMU YA VIII: MASHARTI YA JUMLA

**35. Kizuizi**

Hakuna yeyote atakaye-

a) Zuia afisa wa kundi la usimamizi wa ufuo kutekeleza kazi rasmi katika eneo lake la mamlaka kulingana na masharti katika kanuni hizi; au
b) Kukataa au kukosa kujibu maswali yoyote, au kutoa habari yoyote au kutoa hati yoyote muhimu katika masharti ya kanuni hizi atakapotakiwa kufanya hivi na mwanachama yeyote wa kamati tendaji au afisa wa uvuvi aliyeidhinishwa.

**36. Uharibifu mbaya wa hati za Kundi la Usimamizi wa Ufuo**

Hakuna yeyote atakaye tumia njia ya udanganyifu au kubadilisha, kuharibu, kufuta tamko lolote, cheti, lebo ya utambulisho au hati yoyote iliyotengenezwa au kutolewa kulingana na hizi kanuni.

**37. Adhabu**

Yeyote atakayekiuka masharti ya kanuni hizi atakuwa na hatia na kuwajibika kutozwa faini isiozidi shilingi laki moja au kifungo kisichozidi miaka miwili au yote mawili.

## RATIBA

RATIBA YA KWANZA
Sheria Za Uvuvi
[Cap. 378]
KANUNI ZA UVUVI (KUNDI LA USIMAMIZI WA UFUO)

RATIBA YA PILI
Sheria Za Uvuvi
[Cap. 378]
KANUNI ZA UVUVI (KUNDI LA USIMAMIZI WA UFUO), 2007

RATIBA YA TATU
Sheria Za Uvuvi
[Cap. 378]
KANUNI ZA UVUVI (KUNDI LA USIMAMIZI WA UFUO), 2007

RATIBA YA NNE
Sheria Za Uvuvi
[Cap. 378]
KANUNI ZA UVUVI (KUNDI LA USIMAMIZI WA UFUO), 2007

HII NAKALA IMETAFSIRIWA NA FAZA YOUTH ACTION GROUP IKIDHAMINIWA NA LAMU ENVIRONMENT FOUNDATION.